KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 9, Issue 2

4th Jumaa al-Awwal 1432

8th April, 2011

Yaliyomo

NJIA ZA KUPAMBANA NA... 1 - 2

AMALI NJEMA & FATAWAA 3 - 4

NJIA ZA KUPAMBANA NA FITINA

Mtayarishi: Sheikh Muhammad Saalih al-Munajjid

Kuna tabia fulani ambayo Muislamu anafaa awe nayo pindi anapopambana na fitna ili hizo fitna zisije zikamletea madhara, na ili yeye asilete madhara kwenye Ummah.

BAADHI YA TABIA ZENYEWE:

A. Utaratibu, Upole, kusamehe, na Kutokuwa na Pupa.

Utaratibu, upole na kusamehe wakati wa mitihani na utesi ni athari zenye kupendeza, kwa sababu hayo humwezesha Muislamu kuona mambo kama yalivyo na kuelewa vyema yale yanayo endelea.

Mtume (صلي الله عليه وسلم) amesema: "Hakika upole hauwi mahali popote isipokuwa hurembesha, wala hauondolewi mahali popote isipokuwa hufedhehesha."[Muslim].

Na Mtume (صلي الله عليه وسلم) alimwambia Ashajj' Abdul Qays (رضي الله عنه): "Wewe unazo sifa mbili zipendwazo na Allaah, Upole na Utaratibu." (Muslim)

Kwahivyo sote ni lazima tuwe wapole katika fikra zetu na tabia zetu, na katika mambo yote yanayotokea, na tusiwe ni wenye pupa, kwa sababu hiyo si njia ya Ummah wa ki-Islamu, haswa katika nyakati za fitnah.

B. Subira: Twahitaji mno subira, haswa katika wakati wa fitna. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na Wallaahi tutawafanyia mtihani (ijapokuwa kwa kitu kidogo) mfano wa hofu na njaa, kuondokewa na baadhi ya mali, kufiliwa (na baadhi ya vipenzi) na kuondokewa na baadhi ya matunda (mashamba); na wape habari nzuri wenye kusubiri (kwa pepo). Ambao unapowapata msiba wowote husema hapana shaka sisi ni waja wa Mwenyezi Mungu na hapana shaka kwake yeye ni wenye kurudi. Hao huwateremkia baraka kutoka kwa Mola wao na Rehma, na hao ndio (hakika) walio-ongoka. (BAQARAH:155-157)**

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Tha'labah al-Khushani (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema "Baada yako zitakuja siku za subra (yaani siku zitakazo hitaji subra). Subra siku hizo itakuwa ni kama kushika kaa la moto. Siku hizo thawabu za mtu atakayeshikana na maamrisho ya Allaah itakuwa ni sawa na thawabu za watu hamsini waliofanya kitendo kama chake." Akasema "Ya Rasullallaah malipo ya hamsini wao?" Akajibu Mtume (صلي الله عليه وسلم): "Malipo ya hamsini wenu." (Abu Dawood, Ibn Maajah, imesahihishwa na Albaani kwenye saheehah).

Kukiwa na subra, tafauti baina ya wale walio na bidii na kuamini na wale walio waoga na udhaifu hudhihirika. Kwahivyo Salafus-Swaalih walifahamu umuhimu wa subra nyakati za mitihani na mambo mapya yanayo tokea. Hapa kuna baadhi ya mifano inayotokamana na visa vya maisha yao:

Wakati Maswahaba (رضي الله عنهم) walipokuwa wakinyanyaswa na kuteswa wakati wa mwanzo wa Uislamu Makkah, Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa akiwapitia na kuwakumbusha wawe na subra.

Alipopita kwa familia ya Yaasir (رضي الله عنه) alikisema "Kuweni na subra O ali Yaasir, hakika mmeahidiwa Jannah". (imesahihishwa na Albani kwenye Takhreej Fiqh al-seerah, Uk.103)

Imehadithiwa kuwa az-Zubayr ibn 'Adiyy alisema: "Tulikuja kwa Anas ibn Maalik na tukalalamika kwake kuhusu mateso tunayoyapata kutoka kwa al-Hajjaaj. Akasema "Kuweni na subra, hautokuja wakati ila ufuatao ni muovu zaidi, mpaka mtakapokutana na Mola wenu." Nilisikia haya kutoka kwa Mtume wenu (صلي الله عليه وسلم) (Bukhari)

Al-Mustawrid al-Qurashi alimwambia 'Amr ibn al-'Aas (رضي الله عنه): "Nilimsikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema, "Kiyamah kitasimama wakati Warumi ndio watakaokuwa watu wengi.'" Amr akasema, "Chunga unayoyasema". Akasema "Nasema niliyoyasikia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) . Amr akasema, "Ikiwa wasema hivyo, basi ni hakika, kwani wao (Warumi) wana sifa sampuli Nne. Wao ndio wenye subra mno wakati wa fitnah kuliko watu wote, warudisha hali zao kwa upesi baada ya msiba; ni wepesi kurudi hali zao na kushambulia tena na kushinda, na ni wema kwa maskini, mayatima na madhaifu. Na sifa ya tano walio nayo wanapambana na dhulma za wafalme." (Muslim).

Al-Nu'maan ibn Basheer alisema: "Ikiwa hakuna kilobakia ulimwenguni ila mitihani na fitnah, basi ikabili mitihani kwa subra."

Wakati Imam wa Ahl al-Sunnah wa'l-Jamaa'ah, Ahmad ibn Hanbal, alipokabiliwa na fitnah kubwa ya wale waliosema kuwa Qur'an

NJIA ZA KUPAMBANA NA FITINA

imeumbwa, wakati wa utawala wa al-Mu'moon, al-Mu'tasim na al-Waathiq, wakati alipofungwa jela mda mrefu ni kichapo kibaya, aliyachukua hayo yote kwa subra na kushikamana na Dini yake njia ilio nyoka, mpaka Allaah akampa ushindi na afueni kutoka kwenye mateso hayo.

C. UADILIFU NA USAWA KATIKA MAMBO YOTE:

Sababu kubwa za kukhitilafiana watu, haswa nyakati za fitnah, ni ukosefu wa Uadilifu na Usawa. Ikiwa Muislamu atafanya juhudi awe na usawa kwa nafsi yake na kwa wengine, basi mengi ya matatizo yatokeyao baina ya Waislamu, yakiwa ni kwenye daraja ya Umoja au wengi, yatatatuliwa insha-Allaah. Allaah akasema: **"Na kila ukitoa neno lako sema haki" (al-An'aam:152). "Na usikubali uadui na chuki za wengine....." (al-Maidah:8**). Kwahivyo ni muhimu kuwa waadilifu katika maneno na vitendo vyetu, haswa wakati wa fitna, katika kuangalia kwa busara kila jambo na kupima mema na maovu yake, kisha tutoe hukumu, kwa sababu tukiyapima mambo vizuri tutawahami Waislamu katika kuyanasibisha mambo kwa Uislamu yasio maamrisho ya Allaah. Kwa hivyo uadilifu wako na usawa wakati wa fitnah utakuokoa inshaAllaah.

Sheikh Muhammad ibn Saalih al-Uthaymeen (رحمه الله) alisema:

"Nawahimiza Enyi ndugu zangu muwe na uadilifu na kipimo cha Usawa katika mambo yote, katika mtazamo wenu kulihusu jambo lolote, kupata hukmu ya usawa kuyahusu, na kuhukumu mambo yote kwa sampuli moja. Hili ni jambo muhimu ambalo mtu wa busara hulifuata katika uhusiano wake na Allaah na wengine kwa kuwa mtu wa usawa. Allaah anawapenda wenye kufanya usawa. Unafuata mfano kutoka kwa Salafus-Swaalih katika bidii yao yakuwa waadilifu na wenye usawa: Ilihadithiwa kuwa 'Abd al-Rahman ibn Shimaasah aliyesema: "Nilikuja kwa Aa'isha (رضي الله عنها) nikamuuliza kuhusu kitu, akasema, wewe ni mtu wa kutoka wapi?" Nikasema, "Mimi natoka Misri." Akasema, "Tabia ya hakimu wenu (governor) ilikuwa vipi katika vita vyenu hivi?" Nikasema "Hatukuona jambo baya kutoka kwake. Ikiwa ngamia wa mmoja wetu alikufa atakupa mwengine. Ikiwa yoyote amepoteza mtumwa wake, atakupa mtumwa mwingine. Ikiwa mtu anamahitaji ya mambo ya kawaida, atawapa nafaka." Akasema mambo aliotendewa ndugu yangu Muhammad ibn Abi Bakr, hainizuwii kukuambia yale niliyoyasikia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) Alisema kwenye nyumba yangu hii: 'O Allaah yoyote atakayepata utawala juu ya mambo ya watu wangu na akawa mgumu kwao, basi O Allaah kuwa mgumu kwake, na yoyote atayepata utawala juu ya mambo ya watu wangu, akawa mwema kwao, basi kuwa mwema kwake." (Muslim)

Katika kuisherehesha hadeeth hii, Imaam an-Nawawi (رحمه الله) alisema: "Hi yaonyesha kuwa twafaa tuyataje mambo mazuri ya watu wazuri, na kutojizuia na kufanya hivyo. Wakikhitilafiana kuhusu alivyouliwa Muhammad huyu. Yasemekana kuwa aliuawa vitani na yasemekana kuwa aliuawa baada yakuchukuliwa mateka. Mtawala anayetajwa hapa ni Mu'aawiyah ibn Hudayj aliye muuwa Muhammad ibn Abi Bakr." [Al-Siyar, 3/38]. Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

NENO LA BUSARA

Amesema Mtume (صلي الله عليه وسلم):

"

Hawatovurumizwa watu motoni kwa nyuso zao – au kwa pua zao – isipokuwa [ni kwa] kutokana na mavuno ya ndimi zao?

"

Sheikh Abdul-Muhsin al-'Abbaad

MFANO WA AMALI NJEMA TUWEZAZO KUTENDA KUONGEZA HASANAAT

Na Sheikh al-Munajjid

Alhamdulilah Rabi al-Alameen.

Ikiwa Allaah (سبحنه وتعلي) atamsaidia Muislamu kufanya amali njema, basi aweza kupata thawabu nyingi. Kuna amali njema za sampuli nyingi ambazo zaweza kutendwa na tajiri, maskini, mzee, kijana, mume na mke kulingana na hali ya bidii na uwezo wa kila mmoja, baada ya msaada wa Allaah. Allaah amesema: **"Atakaefanya mema miongoni mwa mwanamume au mwanamke ilihali ni mwenye muamini, Wallaahi tutampa, tutampa maisha mazuri na hakika tutamlipa malipo yake kwa uzuri wa waliyokuwa wakiyafanya."** [**al-Nahl:97**]

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema "Fanyeni bidii katika kufanya amali njema kabla hayajafika majanga kama vipande vya giza la usiku, wakati mtu atakapo kuwa muumim asubuhi na akawa kaafir jioni, au awe muumin jioni na kaafir asubuhi, akiuuza majukumu ya dini yake kwa mapato ya kilimwengu". Mfano wa amali njema ambazo mtu aweza kutenda kila siku ni kama zifuatazo:

1-**KUSWALI KWA JAMAA'AH MSIKITINI:**

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema "Yoyote atakayekwenda msikitini asubuhi na jioni, Allaah atamtayarishia mahali patukufu katika Jannah kila akienda na kuja." [al-Bukhari & Muslim].

2-**KUHUDHURIA MAZISHI NA KUMSWALIA MAITI:**

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: "Yoyote

MFANO WA AMALI NJEMA TUWEZAZO KUTENDA KUONGEZA HASANAAT

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

atakayehudhuria mazishi mpaka akamswalia maiti atakuwa na qira'at kimoja (Ya malipo) na atakayehudhuria mpaka maiti akesha kuzikwa atakuwa na qira'at viwili." Ikasemwa ni nini qira'at viwili? Akasema **(**صلي الله عليه وسلم**)**: "Ni kama milima miwili mikubwa". [al-Bukhari & Muslim]

3-KUSEMA *"LAA ILAAHA ILLALLAAH WAHDAHU LAA SHAREEKA LAH, LAHUL-MULK WALAHUL HAMD WAHUWA 'ALAA KULLI SHAY-IN QADEER."* mara mia kila siku.

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah **(**رضي الله عنه **)** kuwa Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** alisema "Yoyote atakaye sema '*Laa ilaaha ill-Allaah wahdahu laa shareeka lah, lahu'l-mulk wa lahu'l hamd wa huwa 'ala kulli shay'in qadeer'*" mara mia kwa siku, itakuwa ni kama amewaacha huru watumwa kumi na hasanaat mia ataandikiwa yeye (mazuri) na sayiaat mia atafutiwa (maovu) na itakuwa kinga kwake na shaytaan siku mzima mpaka jioni ikija. Hakuna awezae kufanya uzuri zaidi ila yule atakayefanya zaidi." [al-Bukhari & Muslim].

4-KUSHIKANA NA AR-RAHM (kizazi):

Imehadithiwa kutoka kwa Anas **(** رضي الله عنه **)** kuwa Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** alisema "Yoyote atakayeriziki yake iongezeke na umri wake kuongezwa basi na ashikamane na kizazi" [al-Bukhari & Muslim].

5-KUFUNGA SWAUMU ZA SUNNAH, KUTEMBELEA WAGONJWA NA KUTOA SWADAQA:

Ilihadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah **(**رضي الله عنه**)** yakwamba alisema Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)**: "Ni nani katika nyinyi leo aliyefunga ?" Abu Bakr **(**رضي الله عنه **)** akasema: "Mimi". Akasema **(**صلي الله عليه وسلم**)**: "Ni nani katika nyinyi aliyehudhuria mazishi leo?" Abu Bakr **(**رضي الله عنه **)** akasema: "Mimi." Akasema **(**صلي الله عليه وسلم**)**: "Ni nani katika nyinyi aliye mlisha masikini leo?" Abu Bakr **(**رضي الله عنه **)** akasema: "Mimi". Akasema **(**صلي الله عليه وسلم**)**: "Nani katika nyinyi aliyemtembelea mgonjwa leo?" Abu Bakr **(**رضي الله عنه **)** akasema: "Mimi". Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** akasema: "Mambo haya hayajumuiki pamoja kwa mtu ila itaingia peponi." [Muslim]

6-KUSEMA SUBHAANALLAAH WA BIHAMDIH mara mia:

Ilihadithiwa kutoka kwa Abu Hurayrah **(**رضي الله عنه**)** yakwamba alisema: Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** amesema: "Yoyote atakayesema '*Subhaan Allaah wa bi hmdih'*, mara mia asubuhi na jioni, atafutiwa madhambi yake hata yakiwa kama povu la bahari." [al-Bukhari & Muslim].

7-TASBEEH, TAHMEED, NA TAKBEER, KUAMRISHA MEMA NA KUKATAZA MAOVU NA KUSWALI DHUHAA:

Imehadithiwa kutoka kwa Abu Dharr **(** رضي الله عنه **)** kuwa Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** alisema: "Kwa kila mfupa wa mwana Adam ni lazima sadaka itolewe kila siku. Kila tasbeehah ni sadaka, kila tahmeedah ni sadaka, kila tahleelah ni sadaka, kila takbeerah ni sadaka, kuamrisha mema ni sadaka, kukataza mabaya ni sadaka, na rak'ah mbili zinazoswaliwa asubuhi ya kati na kati (dhuhaa) yatosha."[Muslim].

8-KUSOMA QUR'AN:

Ilihadithiwa kuwa 'Abd-Allaah ibn Mas'ood **(**رضي الله عنه **)** alisema kuwa Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** alisema: "Yoyote atakayesoma herufi moja katika kitabu cha Allaah ataandikiwa jambo zuri na jambo zuri laandikiwa thawabu kumi. Sisemi Alif-Laam-Meem ni herufi, bali Alif ni herufi na Laam ni herufi na Meem ni herufi." Vilevile yako mengi mazuri ambayo Muislamu anafaa kumuomba Allaah **(**سبحنه وتعلي**)** amsaidie kufanya mema na awe na bidii ya kuyatenda hayo. Awe ni mwenye kudumu katika kuyafanya mema hata yakiwa madogo, kwani hivyo ni bora kuliko kufanya makubwa kisha kuacha. Imehadithiwa kuwa Aa'ishah **(**رضي الله عنها**)** alisema: Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** alisema: "Enyi watu fanyeni mazuri muyawezayo, Allaah hachoki kulipa thawabu mpaka mchokapo. Na jambo zuri alipendalo Allaah ni lile analodumu nalo mtu hata kama ni dogo. Ikiwa familia ya Muhammad **(**صلي الله عليه وسلم**)** yaanza kufanya jambo walikuwa wakidumu nalo." [al-Bukhari & Muslim].

HAIJUZU KUANDIKA NENO SALLALLAAHU 'ALAYHI WA-SALLAM KWA UFUPI:

Na Sheikh Ibn Baaz

Twamuomba Allah amfikilizie swala na salaam Mtume wake Muhammad **(**صلي الله عليه وسلم**)**. Waislamu wanawajibika kumswalia na kumtumia salaam Mtume Muhammad **(**صلي الله عليه وسلم**)** wakati jina lake linapotajwa. Allah ametuamrisha **[Hakika Allah na Malaika wake wanamswalia Mtume (**صلي الله عليه وسلم**). Enyi mlioamini! mtumieni swala na salamu kwa ukamilifu]**. Na Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** akasema: [Kila mtu anaponiswalia, Allah amuandikia malipo kumi kwa ajili hiyo] [Ibn Hibaan].

Na Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)** amembainisha mtu ambaye hamswali Yeye akitajwa kuwa ni bakhili wa mabakhili .[Abee 'Aasim]. Na akaitikia Ameen kwa dua ya Jibreel "Mungu amlaani yule ambae asikiapo ukitajwa na asikuswalie" [at-Tabaraani]. Kwa hivyo hapa kuna masala ambayo yataka kubainishwa: Watu wengi hutumia maandishi kwa ufupi "SAW" AU "PBUH" kutimiza wajibu wao wakuandika ,je hili latimiza wajibu wa kumswalia na kumtumia salaam Mtume **(**صلي الله عليه وسلم**)**? Wacha tuangalie baadhi za akwali za Ma-'Ulamaa kuhusu jambo hili.

Kamati ya wanavyuoni wakubwa wa

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Saudi Arabia wakiongozwa na Sheikh 'Abdul-'Azeez ibn Baaz (رحمه الله) walitoa fatwa ifuatayo: "Sunnah ni kuandika kwa ukamilifu bila ya kukata herufi kwa vile ni sampuli ya ibada katika uandishi wa mtu. Kwa sababu ufupisho haukutumiwa na kuruni tatu za kwanza, wale ambao Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliowashuhudilia wema wao.

Al-Fayrooza-Abaadee alisema: "Si sawa kutumia mifano au ufupisho kuonyesha swala na salaam kama wafanyavyo wavivu na wajinga na hata wanafunzi wanaoandika kwa ufupi badala ya ukamilifu. Ahmad Shaakir alisema "Ni desturi ya upumbavu ya waliokuja baadae kufupisha 'sallallaahu 'alayhi wa sallam.'"

Waseeullah al-'Abbaasee alisema "Haifai kwa ujumla kuandika kwa ufupi swala na salam kama vile asivyo faa katika kutamka.

HEIDH NA TALAKA

Na: Sheikh Muhammad Bin Saalih al-Uthaymeen

Tafadhali hebu tufafanulie shuruti za at-Talaaq ar-Raj'ee. Jee mwanamke aliyeachwa atakaa wapi Eda yake, kwenye nyumba ya mumewe au kwenye nyumba ya jamii yake?

Mwanamke aliyeachwa ni lazima akae Eda yake kwenye nyumba ya mumewe na ni haramu kwa mumewe kumfukuza atoke nyumbani. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na musiwafukuze kutoka katika majumba (ya waume) zao, wala wao (wenyewe) wasiondoke isipokuwa iwapo wao wenyewe watakiri makosa yao ya uzinifu. Na hiyo ni mipaka iliyowekwa na Allaah. Na yoyote atakae kengeuka mipaka ya Allaah, basi kwa hakika atakuwa amejidhulumu nafsi yake."** (at-Talaaq 65:1)

Yanayofanywa na baadhi ya watu wenye kuwafukuza wake zao waliowapa talaka kwenda kwenye nyumba za wazazi wao ni mambo ya makosa na yanakwenda kinyume na amri za Allaah, ambae, hapohapo kwenye aya hiyohiyo, amebainisha hikma ya kumuweka mke katika nyumba ya mumewe kwa kusema: **"Wewe (yule ambae aliyemuacha mkewe) hujui, huwenda pengine Allaah ataleta baadae mambo mapya yapite (yaani; akurudishie ikiwa hiyo ilikuwa ni talaka ya kwanza au ya pili)."** (at-Talaaq 65:1)

Kwahivyo, Waislamu wasiishie kwenye mila zao na kuanza kukandamizana dhidi ya sheriya na mipaka iliyowekwa na Allaah.

Akiwa katika nyumba ya mumewe, anaruhusiwa kujipamba na kuwasiliana na mumewe na anaweza kufanya kila jambo linaloruhusiwa isipokuwa yanyopelekea kwenye kuingiliana na mumewe. Mume atakuwa na haki ya kumrudia kwa kutamka "Sasa mimi nakurudia" au anaweza kufanya hivyo kwa kutekeleza kitendo chenyewe cha kumuingilia kwa niya ya kutaka kumrudia. Amma kuhusu Eda ya mwanamke aliyeachwa, nukta fulani zi lazima zibainishwe:

1. Ikiwa aliwachwa kabla ya kuingiliwa na kabla ya kukaa nae katika faragha yoyote, basi hakutokuwa na Eda kwake. Muda uleule anapomuacha, anaweza kuolewa ikiwa atapendelea hivyo. Na iwapo, kwa upande mwengine, alikuwa nae katika faragha, au alitekeleza kitendo cha kuingiliana nae, basi kutakuwepo na Eda kwake. Eda yake itahusiana na masharuti mengine kama ifuatavyo:

A. Ikiwa atakuwa na mimba, basi Eda yake ni mpaka atakapozaa, bila ya kujali urefu wa muda wa mimba yake. Kwa mfano, anaweza kumpa talaka asubuhi na anaweza kuzaa kabla ya mchana. Kwahiyo, (muda wa) Eda yake utakuwa umekwisha. Anaweza kumpa talaka katika mwezi wa Muharram, na akazaa katika mwezi wa Dhul Hijjah. Eda yake ni miezi kumi na mbili. Hii ni kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) ameibainisha yakwamba Eda ya mwanamke mwenye mimba ni: **"Na kwa wale wenye mimba (ema wakiwa wamewachwa au waume zao wamekufa), Eda zao ni mpaka watakapozaa."** (at-Twalaaq, 65:4)

B. Ikiwa hakuwa na mimba, lakini anaweza kupata heidh, basi Eda yake ni Mihula Mitatu Ya Heidh Kamili **baada** ya kuwachwa, yaani; anaingia mwezini kisha anatwahirika (muhula mmoja), akaingia tena mwezini na kutwahirika tena (muhula wa pili), na hatimae anaingia tena mwezini kwa mara ya tatu na kutwahirika (muhula wa tatu). Eda haitotegemea muda utakaokuwepo baina ya kila muhula. Ikiwa, kwa mfano, atawachwa haliyakuwa alikuwa akinyonyesha, na hakupata heidh mpaka baada ya miaka miwili, basi atakuwa bado yuko kwenye Eda, mpaka apate mihula miwili mengine ya heidh. Bila ya kujali kuhusu muda utakaokuwepo baina ya mihula mitatu (mifupi au mirefu) Eda itabakia kuwa ni Mihula Mitatu Kamili, kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wanawake walioachwa watasubiri (kuhusiana na kuolewa kwao) kwa mihula mitatu."** (al-Baqarah 2:228)

C. Ikiwa hana heidh, ema ni mdogo hajafika umri wa kuwa na heidh au ni mkongwe ashapindukia umri wa heidh, basi Eda yake itakuwa ni miezi mitatu kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wale waliokoma na kutoka heidh miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka (katika muda wao wa eda), basi muda wa eda yao ni miezi mitatu (isipokuwa katika hali ya kifo), na (pia ndiyo eda kwa wale) ambao hawajapata heidh bado."** (at-Twalaaq 65:4).

D. Iwapo, kwa sababu zinazojulikana, heidh ya mwanamke aliyekuwa akiendelea kupata imesimama, na wala heidh yake hiyo isimrudie tena (kwa mfano, ameondolewa fuko lake la uzao), basi eda yake ni kama ile ya mwanamke ambaye aliyepitisha umri wa ada ya kila mwezi <u>yaani: miezi mitatu.</u>

E. Iwapo, kwa sababu zinazojulikana, alikosa kupata heidh yake, basi ni lazima asubiri mpaka ile sababu iondoke na heidh yake irudi (kama ilivyokuwa). Eda yake itakuwa ni mihula mitatu kamili.

F. Iwapo, kwa sababu zisizoeleweka, alikosa kupata heidh yake, basi kulingana na wanavyuoni wa Ki-Islamu, atalazimika kukaa Eda ya mwaka mzima: Miezi tisa ya kufidia muda wa kuhimili mimba na Eda ya miezi mitatu.

Hatimae mwanamke ambaye ndoa yake ilimalizika kwa Khul' (kumuacha mke baada ya kulipa kikombozi cha halali kwa mumewe) au kwa njia nyengine, basi eda yake itakuwa ni muhula mmoja.